# MWONGODHO WA MWALIMU
# GIREDI 2

Yumna Hamid Titi
Fuad Aroi
Yumbe Athman

TWAWEZA COMMUNICATIONS
Working Towards a Better World

Shungwaya Welfare Association
Umoja ni Nguvu

SWAHILI RESOURCE CENTRE
Old Town, Sir Mbarak Hinawy Road, Mombasa

Kimechapishwa na:

Twaweza Communications Ltd.
Jumba la Twaweza, Barabara ya Muthithi
Mpesi Lane
S.L.P. 66872 - 00800 Nairobi, Kenya
Simu: +(254) 020 269 4409; 0727 427740
Barua pepe: info@twawezacommunications.org
Wavuti: www.twawezacommunications.org

©Haki a kunakili nḏa Twaweza Communications
Chapisho la Kwanḏa 2024

**ISBN: 978-9966-128-20-1**

Kitabu cha *Chusomeni Kibajuni* ni sehemu a nradi wa kulindra na kuimarisha uṯamaduni wa Vabajuni. Nradi huu huṯekeledhwa na kichuo cha Twaweza Communications, Shungwaya Welfare Association na Swahili Resource Centre. Undofadhiliwa na nfuko wa British Council Protection Fund kwa ushirikiano na Department for Digital, Culture, Media and Sport.

In partnership with

# Yaliyomo


1. Sikuli . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1

2. Sikuli . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 7

3. Mayi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 13

4. Uswafi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 18

5. Usalama . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 24

# SHUKURANI

Dhiṯabu dha *Chusomeni Kibajuni* ni sehemu a juhudi a kulindra na kuimarisha uṯamaduni wa Vabajuni. Chwatoa shukurani kwa mfuko wa British Council Protection Fund kwa nsaada ulochuwedhesha kuanḏika na kuchapisha dhiṯabu hidhi. Bila nsaada wavo ingalikuva ṯabu sana kuvapa vana va Kibajuni nafasi a kuifundrisha kusoma na kuanḏika Kibajuni. Chwavashukuru Dkt. Rukiya Harith na Nafisa Awadh kwa ushirikiano wavo na vaanḏishi kachika haṯua dhoṯe dha kuanḏika nfulululidho wa *Chusomeni Kibajuni*. Vaandishi va dhiṯabu hidhi – Yumna, Aroi na Yumbe – valiiṯolea kushiriki na kumalidha kuanḏika. Chwavashukuru sana kwa nchango huu muhimu. Pia twavashukuru vale voṯe chufanyao navo kadhi hii adwimu a kuhifadhi na kuimarisha uṯamaduni wa Vabajuni.

Kimani Njogu, Twaweza Communications
Omar Lali, Shungwaya Welfare Association
Athman Lali Omar, Swahili Resource Centre

Novemba, 2023

# 1 SIKULI

## ISOMO LA KWANḎA

### MAḎA KURU: KUSIKIDHA

### MAḎA NDRODI: KUANḎAMA MAAGIDHO

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

- Kuanḏama maagidho
- Kufurahia kusikidha maagidho kwa udhuri

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ukurasa wa 1

**Dhifaa dha kufundrishia:** Chati, kifaa cha kidijitali.

**Swali ḏaḏisi**: Kwa nini chuanḏame maagidho?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Changulidha kipindri kwa kuvavulidha vanafunḏi vachaye shuhuli dhifanyikadho sikuli.
- Angika chati ubavoni na uvavulidhe vachambue ni nini vavonacho.
- Vambie vafungue dhiṯabu dhavo ukurasa wa 1, na vasikidhe maagidho a mwalimu.
- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi kuangalia picha kweṉe kifaa cha kidijitali na avaagidhe vaanḏame maagidho kulingana na picha vavonadho.

## ISOMO LA PILI

## MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA

### MAḎA NDRODI: KUṮOA MAAGIDHO

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

- Kuṯoa maagidho
- Kuimba wimbo kwa udhuri

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk 2

**Dhifaa dha kufundrishia:** Dhifaa halisi km. kamba

**Swali ḏaḏisi**: Ni shuhuli gani dhifanyikadho darasani?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

– Changulidha kipindri kwa kuvaambia vanafunḏi vachaye shuhuli dhifanyikadho darasani.

– Mwalimu avaagidhe vanafunḏi vaṯoke inḏe a darasa na aṯoe maagidho ili vaanḏame.

– Vakiva kweṉe dhikundri vanafunḏi vauke kamba.

– Mwalimu avashirikishe vanafunḏi vaimbe wimbo kweṉe uk wa 2.

– Vanafunḏi vaimbe wimbo kwa sauti huku vakiuka kamba.

– Kachika makundri, mwalimu avaagidhe vanafunḏi vaṯabe shuhuli mbalimbali dha darasani.

## ISOMO LA CHACHU

## MAḎA KURU: KUSOMA

### MAḎA NDRODI: KUSOMA MICHORO

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

- Kueledha michoro kwa ufasaha.
- Kuchunga senchensi kwa kuchumia michoro.

**Marejeleo:** Kiṯabu cha vanafunḏi uk. 3.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kadi-maneno, chati yenye senchensi.

**Swali ḏaḏisi:** Sikuli hufanywa shuhuli gani?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Changulidha isomo kwa kuvavulidha vanafunḏi shuhuli vafanyadho darasani.
- Mwalimu atoe kadi-maneno, vanafunḏi vadhisome.
- Vaagidhe vafungue dhiṯabu ukurasa wa 3 ili vaenge michoro na vaeledhe vavonacho.
- Mwalimu achunge senchensi akichumia michoro.
- Vaagidhe vanafunḏi vachunge senchensi vakichumia michoro ilioko kweṉe kitabu uk wa 3.
- Hitimisha isomo kwa kuvashirikisha vanafunḏi vasome senchensi kweṉe chati.

**ISOMO LA IṈE**

**MAḎA KURU: KUSOMA**

**MAḎA NDRODI: KUSOMA KIFUNGU**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe.

- Kusoma kufungu cha hadisi kwa udhuri.
- Kujibu maswali a kifungu cha haḏisi.
- Kufurahia kusoma

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi uk. wa 4

**Dhifaa dha kufundrishia:** Dhifaa halisi dha darasani

**Swali ḏaḏisi:** Darasani hupachikana dhichu gani?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

– Changulidha isomo kwa kuvavulidha vanafunḏi vachaye dhichu dhipachikanadho darasani.

– Vavoneshe dhifaa halisi darasani kama ubavo, ibavo la kukeṯia, choki nk.

– Vaekedhe vanafunḏi ukurasa wa 4 ili vajaḏili michoro iliyoko kiṯabuni.

– Mwalimu asome kifungu kwa sauṯi na avape muḏa vanafunḏi vasome kimwa kimwa.

– Avaagidhe vanafunḏi vasome kifungu kwa sauti na aṯaue mwanafunḏi mmoya mmoya asome kwa sauṯi.

– Vape muḏa wa kujibu maswali a kifungu kachika dhiṯabu dhavo.

– Hitimisha isomo kwa kuvapa vanafunḏi nafasi a kuṯoa ufupisho kuhusu kifungu valichokisoma.

**Majibu alopendekedhwa:**

1. Sikuli a Kaa Chonjo.

2. Bakora

3 a) Hana bidii/ ndhivu

b) Hungia sikuli kuchelewa

4. La, si nduri

5. Halisikii dawa

6. Kuva na bidii

## ISOMO LA ṮANU

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: KUANḎIKA MAINA A DHICHU DHA SIKULI

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

- Kuanḏika maina a dhichu kweṉe michoro
- Kuchunga senchensi kuchumia nchoro.

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk 6

**Dhifaa dha kufundrishia:** kadi-maneno.

**Swali ḏaḏisi:** Ni dhichu gani hupachikana sikuli?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Changulidha isomo kwa kuvavonesha dhichu darasani kama kichi, kiṯongoo, medha na uvambie vadhichambue.
- Vashirikishe kuchunga senchensi vakichumia maina a dhichu hidho.
- Vambie vafungue kiṯabu cha mwanafunḏi uk wa 6. Vakiva vavili vavili vachambue na kujadili picha dhilidhoko kiṯabuni.
- Vanafunḏi vaeledhanye dhichu hidho na vachaye maina.
- Vashirikishe kuchunga senchensi vakichumia maina hao.

## ISOMO LA SIṮA

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: HARUFU KURU NA NDRODI

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

- Kuanḏika senchesi kwa harufu kuru na ndrodi.
- Kufurahia kuanḏika.

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk 7.

**Dhifaa dha kufundrishia:** kadi-maneno.

**Swali ḏaḏisi:** Ni maneno gani ladhima aandwe kwa harufu kuru?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Changulidha kipindri kwa kuvaagidha vanafunḏi kusoma harufu a-z kwa sauṯi.
- Toa mifano ubavoni iloandikwa kwa harufu ndrodi na kubadilisha kwa harufu kuru.
- Vashirikishe vaanḏike senchensi ubavoni kwa harufu kuru na ndrodi.
- Toa kadi-maneno dha harufu kuru na ndrodi ili vanafunḏi vachambue na kudhisoma.
- Hitimisha isomo kwa kuvaagidha vanafunḏi vajibu maswali ukurasa wa 7.

**Majibu alopenḏekedhwa**:

1. MWALIMU ALIANḎIKA UBAVONI

2. SIKULI ECHU INA UVANḎA NKURU

3. MWANAFUNḎI HODARI HUPAWA DHAWAḎI

1. kalamu angu inḏopotea.

2. mwalimu husomesha kwa udhuri.

3. mabuku aliraruka.

# 2 SIKULI

## ISOMO LA KWANḎA

**MAḎA KURU: KUSIKIDHA**

**MAḎA NDRODI: KUANḎAMA MAAGIDHO**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

- Kueledha maagidho apawao.
- Kuanḏama maagidho

**Swali ḏaḏisi**: Mwalimu hutoa maagidho gani sikuli?

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi ukurasa wa 8

**Dhifaa dha kufundrishia**: chati, kadi dhenye maagidho

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi kueledha kuhusu picha dhiṯabuni uk. 8.
- Kachika makundri mwanafunḏi mmoya aeledhe vangine vasikidhe kwa makini.
- Vanafunḏi vasome maagidho kachika kadi dha maneno na vaandame.
- Mwalimu avashirikishe kachika ntedho wa kupichisha ujumbe kuṯoka kwa nchu mmoya hadi nngine kweṉe mashikio kwa siri.
- Vahimidhe umuhimu wa kuva makini vapawapo ujumbe.

## ISOMO LA PILI

## MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA

## MAḎA NDRODI: DHICHANDRAWILI/DHICHONDROVI

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe

- Kuchega na kuchegua dhichandrawili
- Kufurahia kuchega na kuchegua dhichandrawili

**Swali ḏaḏisi**: Dhichandrawili ni nini?

Dhichandrawili hukusudia nini kachika masomo?

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ukurasa wa 9

**Dhifaa dha kufundrishia**: Picha dheṉe kutoa majibu a dhichandrawili.

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Vaeledhee vanafunḏi umuhimu wa dhichandrawili. Kisha vaavanye kachika makundri.
- Vakiva kachika makundri vanafunḏi vakumbusane dhichandrawili vadhiyivadho.
- Vanafunḏi vachegeane dhichandrawili kwa kushindrana.
- Mwalimu avapongedhe vanafunḏi na avahimidhe kukusanya dhichandrawili dhaidi
- Mwisho mwalimu avape dhichandrawili vajibu dhiṯabuni ukurasa wa 9.

**Majibu alopenḏekedhwa**

1. Kiachu
2. Dhichakwi
3. Nocha angani

4. Kishogo

5. Kufuli

6. Kamasi

7. Kobe/fududu

8. Nlango

9. Kope

10. Ulimi na menyo

**ISOMO LA CHACHU**

## MAḎA KURU: KUSOMA

**MAḎA NDRODI: KUSOMA SENCHENSI**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

- Kusoma senchensi kwa kudhingatia silabi.
- Kuanḏika senchensi kwa udhuri.
- Kufurahia kusoma na kuanḏika senchensi.

**Swali ḏaḏisi**: Ni siku gani hupandrishwa bendera sikuli?

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk 9

**Dhifaa dha kufundrishia**: kadi-maneno, chati eṉe senchensi

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Vashirikishe vanafunḏi kusoma kadi maneno kachika dhikundri.
- Vanafunḏi vaundre senchensi na kudhisoma.
- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi kusoma senchensi validhodhiundra kuchumia kadi-maneno.

- Vanafun̲di vasome kwa pamoya senchensi dhilidho kit̲abuni ukurasa wa 9.
- Vanafun̲di vashindrane kusoma senchensi dhit̲abuni.

## ISOMO LA IN̲E

## MAD̲A KURU: KUSOMA

**MAD̲A NDRODI: KUSOMA KIFUNGU**

**Mat̲okeo maalumu t̲arajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafun̲di awedhe:

- Kusoma kifungu kwa udhuri na kwa kasi.
- Kujibu maswali a kifungu.

**Swali d̲ad̲isi**: Ni vanafun̲di gani hudhawad̲iwa?

**Marejeleo**: Kit̲abu cha mwanafundi ukurasa wa 10 – 11

**Dhifaa dha kufundrishia**: chati, picha kit̲abu cha mwanafun̲di ukurasa wa 10.

**Ut̲arat̲ibu wa kufundrisha**

- Vaongodhe vanafun̲di kudhungumudha kuhusu picha kachika kit̲abu cha mwanafun̲di ukurasa wa 10.
- Vanafun̲di vasome kifungu kimwa kimwa kisha vasome kwa saut̲i.
- Mwalimu avakumbuse kuan̲d̲ama maad̲ili madhuri a kusoma.
- Vanafun̲di vachambue maneno magumu.
- Vaeledhe maana a maneno hao.
- Mwalimu avape maswali vanafun̲di vajibu dhit̲abuni.
- Vahimidhe kusoma dhaidi n̲umbani.

**Majibu alopenḏekedhwa**

1. Shuhuli a siku a dhawaḏi.

2. Valofanya udhuri kachika nṯihani.

3. a) Dhawaḏi dha alopacha alama nḏuri.

   b) Mwanafunḏi mweṉe aḏabu.

   c) Mwanafunḏi nsafi.

4. Kusikilia sikuli mapema.

5. Peche

## ISOMO LA ṮANU

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: KUANḎIKA SENCHENSI

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

- Kuanḏika senchensi kwa haṯi nḏuri
- Kusoma senchensi
- Kufurahia kuanḏika na kusoma senchensi

Kusoma senchensi

**Swali ḏaḏisi**: Ni mambo gani afanywao sikuli?

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ukurasa wa 12.

**Dhifaa dha kufundrishia**: Chati, kadi-maneno.

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Vaavanye vanafunḏi kachika makundri. Vanafunḏi

vadhungumudhe vavonacho kweṉe picha dhiṯabuni uk. 12

- Vanafunḏi vasome maneno kweṉe kadi vashikanishe kadi kuundra maneno.
- Vanafunḏi vachunge senchensi kisha vadhisome.
- Vanafunḏi vaandike kwa haṯi swafi kuhusu kisa kitokanacho na michoro kiṯabuni uk.12.

## ISOMO LA SIṮA

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: KUANḎIKA SENCHENSI

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

- Kuchunga senchensi kwa kupanga maneno sawa.
- Kusoma senchensi.

**Swali ḏaḏisi:** Senchensi nduri huundrwaye?

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi, ukurasa wa 13.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kadi-maneno.

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Vakumbuse vanafunḏi namuna a kuundra maneno kwa kuchumia harufu
- Kachika dhikundri vanafunḏi vachumie kadi dha maneno kupanga senchensi vadhisome.
- Vanafunḏi vavonyeshe senchensi dhavo mbee a darasa.
- Vaongodhe kufanya dhoedhi ukurasa wa 12.
- Vanafunḏi vasome kwa sauṯi.

# 3 MAYI

## ISOMO LA KWANḎA

**MAḎA KURU: KUSIKIDHA**

**MAḎA NDRODI: NGANU**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

- Kusikidha nganu kwa makini.
- Kuchambua alioko kachika michoro.

**Maswali ḏaḏisi**: Mayi husaidia nini?

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk 14.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Dhiṯabu dha nganu.

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha:**

- Vashirikishe vanafunḏi kudhungumudha kuhusu nganu. Vaeledhee kuhusu picha.
- Mwalimu avasomee vanafunḏi nganu kachika kiṯabu cha nganu kwa kuchumia lugha a Kibajuni.
- Vanafunḏi vachambue umuhimu wa mayi kuṯoka kweṉe nganu.
- Vashirikishe vanafunḏi kudhungumudha kuhusu umuhimu wa mayi.
- Vahimidhe vanafunḏi kuchaya umuhimu wa mayi na nḏia dha kuhifadhi mayi.

## ISOMO LA PILI

## MAḎA: KUDHUNGUMUDHA

**MAḎA NDRODI:–KUHIFADHI MAYI**

**Maṯokeo maalum ṯarajiwa**: Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

- Kuchaya nḏia dha kuhifadhi mayi
- Kueledha machumidhi mbalimbali a mayi

**Swali ḏaḏisi:** Mayi hupachikana kwapi?

Mayi chuchumiao ṉumbani hutoka kwapi?

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk. 15

**Dhifaa dha kufundrishia:** michoro, chati

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Vashirikishe vanafunḏi kuchaya mambo kuhusu picha dhiṯabuni uk 15.
- Kachika dhikundri vanafunḏi vajaḏili nḏia dha kuhifadhi mayi.
- Mwalimu avasikidhe vanafunḏi vakijaḏiliana kisha avaandikie ubavoni, vanafunḏi vasome nḏia dha kuhifadhi mayi.
- Vashirikishe vanafunḏi kuchaya nḏia dha kuhifadhi mayi dhilidhoko dhiṯabuni kama jabia, kisima, miṯungi n.k.

## ISOMO LA CHACHU

## MAḎA: KUSOMA

**MAḎA NDRODI: UFAHAMU**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe;

- Kuchambua umuhimu wa mayi.
- Kubainisha aina mbalimbali dha mayi.

**Swali ḏaḏisi:** Mbona mayi ni uhai?

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk 15.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kadi maneno, kadi dha picha.

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Vakumbuse vanafunḏi kuhusu somo lilopicha kuhusu mayi.
- Vanafunḏi kachika dhikundri vasome ufahamu. Vachambue nḏia dha kuhifadhi mayi.
- Vanafunḏi vachaye umuhimu wa mayi ṉumbani, mashambani na haṯa kwa nvili wa mwanadamu.
- Vanafunḏi vachaye umuhimu wa mayi, vaṯabe shuhuli dha kuchumia mayi.

**Majibu alopenḏekedhwa:**

1. Zingatia jibu la mwanafunḏi
2. Ndrio
3. Kweṉe jabia, mitungi, mapipa
4. Haitoi madhao madhuri
5. Kusaga chakula, kupungudha jocho, kung'arisha ngodhi

**ISOMO LA IṈE**

## MAḎA: KUSOMA

**MAḎA NDRODI: KUSOMA SENCHENSI**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

- Kusoma senchensi kwa ufasaha.
- Kufurahia kusoma senchensi.

**Swali ḏaḏisi:** Nsomi ndhuri ni upi?

Ni nini husaidia kusoma kwa udhuri?

**Marejeleo:** Kitabu cha mwanafunḏi cha 2 uk.16

**Dhifaa dha kufundrishia**: Kadi-maneno, kadi dha senchensi

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Vavoneshe vanafunḏi kadi dha maneno. Vasomee na vanafunḏi varudie.
- Mwalimu avape vanafunḏi kadi dha maneno vachambue na vasome kwa sauṯi.
- Vanafunḏi vashikanishe kadi dha maneno vaundre senchensi kisha vasome senchensi kwa sauṯi.
- Vanafunḏi vasome senchensi dhiṯabuni kwa sauṯi.

## ISOMO LA ṮANU

## MAḎA: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: KUUNDRA MANENO

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe;

- Kupanga harufu kuundra maneno.
- Kusoma maneno kwa udhuri
- Kufurahia kupanga na kusoma maneno

**Swali ḏaḏisi:** Maneno hundrwae?

**Marejeleo:** Kiṯabu cha Mwanafunḏi uk 17.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kadi dha harufu.

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Mwalimu avape vanafunḏi kadi dha harufu kachika dhikundri.
- Vanafunḏi vadhichumie harufu hidho, vadhichambue harufu hidho kachika maneno.
- Vanafunḏi vaandike maneno dhiṯabuni na vasome kwa sauṯi.
- Mwalimu avashirikishe kukamilisha dhoedhi dhiṯabuni.

**Majibu alopenḏekedhwa:**

| | |
|---|---|
| 1. kuosa | 2. kisima |
| 3. jabia | 4. kukoa |

| | |
|---|---|
| 5. dhombo | 6. kufua |
| 7. kunyava | 8. ntungi |
| 9. kunwa | 10. idovo |

**SOMO LA SIṮA**

## MAḎA: KUANḎIKA

**MAḎA NDRODI: KUUNDRA MANENO**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

- Kuundra maneno kuṯoka kwa jedwali.
- Kusoma maneno
- Kufurahia kuundra maneno.

**Swali ḏaḏisi:** Silabi ni nini?

- Ineno huundrwae?

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi uk 17

**Dhifaa dha kufundrishia:** Jedwali, kadi za silabi.

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Chumia kadi dha silabi kuvachambulisha vanafunḏi silabi ni nini?
- Vaongodhe vanafunḏi kuundra maneno kwa kuchumia silabi mbalimbali.
- Vasome silabi na vaunganishe kupacha maneno sawa.
- Vanafunḏi vasome silabi kweṉe jedwali vashindrane kupacha maneno kuchumia jedwali.
- Vanafunḏi kachika dhikundri vaandike maneno kuṯoka jedwali.
- Vanafunḏi vasome maneno valoundra kwa sauṯi.

# 4 USWAFI

## ISOMO LA KWANḎA

**MAḎA: KUSIKIDHA**

**MAḎA: NDRODI: HAḎISI**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe;

- Kusikidha haḏisi kwa makini na kubaini ujumbe.
- Kujibu maswali kutokana na haḏisi.

**Maswali ḏaḏisi:** Uswafi una umuhimu gani?

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk 18

**Dhifaa dha kufundrishia:** Michoro

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Vaeledhe vanafunḏi umuhimu wa uswafi.
- Mwalimu avasomee haḏisi kiṯabuni avaongodhe vanafunḏi kusoma pia.
- Mwalimu avavulidhe maswali vanafunḏi vajibu kuṯoka kwa haḏisi.
- Vaeledhe maana a maneno mapiya.
- Vajibu maswali

**Majibu alopenḏekedhwa**

1. Kuswafi
2. Uswafi wa madhingira
3. Kufanya uswafi

4. N̠umbani, sikuli na choni

5. Chufundrishane uswafi

**ISOMO LA PILI**

## MAD̠A: KUDHUNGUMUDHA

**MAD̠A NDRODI: MADHUNGUMUDHO KUHUSU USWAFI**

**Mat̠okeo maalumu t̠arajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafund̠i awedhe;

- Kusoma madhungumudho kuhusu uswafi.
- Kujibu maswali
- Kufurahia madhungumudho kuhusu uswafi.

**Marejeleo:** Kit̠abu cha mwanafund̠i ukarasa 19

**Dhifaa dha kufundrishia:** Picha

**Ut̠arat̠ibu wa kufundrisha**

- Mwalimu at̠auwe vanafund̠i vavili vat̠abe madhungumudho kachi a mwalimu na mwanafund̠i nchafu.
- Vashirikishe vanafund̠i vasome madhungumudho kit̠abuni uk.19 kachika dhikundri.
- Vanafund̠i vachaye uswafi wa nvili wa kila siku.
- Vanafundi vajibu maswali

Kadhi a dhiada: vanafund̠i vafanye uswafi n̠umbani.

**Majibu alopend̠ekedhwa**

1. Kuhusu uswafi

2. Radhia na Salama

3. Nchafu

4. Radhia

5. Ndriyo, alinfundrisha Radhia kuhusu uswafi

**ISOMO LA CHACHU**

## MAḎA: KUSOMA

**MAḎA NDRODI: SHAIRI**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe;

- Kusoma na kukariri shairi.
- Kutoa ujumbe kutoka shairi
- Kufurahia kukariri shairi

**Maswali ḏaḏisi:** Uswafi una umuhimu gani?

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk 20

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kifaa cha kidijitali

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**:

- Mwalimu avasikidhishe vanafunḏi shairi kwa kuchumia kifaa cha kidijitali
- Vanafunḏi valisome shairi dhiṯabuni kwavo.
- Vanafunḏi valikariri shairi kwa mahadhi.
- Mwalimu avaeledhee maana a maneno magumu
- Vanafunḏi vafurahie shairi, valikariri na kuṯaba.

## ISOMO LA IN̲E

## MAD̲A: KUSOMA

### MAD̲A NDRODI: SENCHENSI

**Mat̲okeo maalumu t̲arajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafund̲i awedhe;

- Kusoma senchensi kwa kuendreledha.
- Kufurahia kusoma senchensi.

**Maswali d̲ad̲isi:** Kuyiva kusoma kuna umuhimu gani?

**Marejeleo:** Kit̲abu cha mwanafund̲i uk 21

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kadi dha senchensi, kadi-maneno

**Ut̲arat̲ibu wa kufundrisha**:

- Vaveke vanafund̲i kwen̲e dhikundri vasome kadi zen̲e maneno.
- Vanafund̲i vasaidiane kuchambua maneno kwen̲e kadi.
- Vashirikishe kupanga kadi-maneno kuchengedha senchensi.
- Vape kadi dhen̲e senchensi vanafund̲i vasaidiane kudhisoma kwa saut̲i.
- Pamoya na vanafund̲i vasome senchensi kachika dhit̲abu dha vanafund̲i.

## ISOMO LA T̲ANU

## MAD̲A: KUAND̲IKA

### MAD̲A NDRODI: HAT̲I ND̲URI

**Mat̲okeo maalumu t̲arajiwa**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafund̲i awedhe;

- Kuand̲ika kwa hati nd̲uri
- Kusoma senchensi

- Kufurahia kuanḏika

**Maswali ḏaḏisi**: Kwa nini chuifundrishe haṯi?

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk. 22

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kadi dheṉe senchensi (haṯi swafi)

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**:

- Vakumbuse vanafunḏi kuhusu harufu, nfano dha kwendra iyu, dha kushuka ṯini na dha kubakia kachi.
- Vashirikishe kuanḏika kwa haṯi nḏuri ubavoni
- Vanafunḏi vashiririkiane kuanḏika ubavoni kwa haṯi nduri.
- Vashirikishe kusoma senchensi hidho na kudhianḏika kiṯabuni

## ISOMO LA SIṮA

## MAḎA: KUANḎIKA

## MAḎA NDRODI: KUUNGANISHA SILABI

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe;

- Kuunganisha silabi kuundra ineno.
- Kusoma ineno.

**Marejeleo:** Kiṯabu mwanafunḏi cha uk. 22

**Swali ḏaḏisi:** Maneno huchengedhwaye?

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kadi-maneno/ harufu.

- Kachika dhikundri vape vanafunḏi kadi zeṉe silabi na harufu
- Vaongodhe vanafunḏi vapange silabi vapache ineno.
- Vaongodhe vanafundi kuundra maneno kuchumia silabi alidhopawa uk.22

- Kachika dhikundri vanafunḏi vavoneshe maneno avo vasome kwa sauṯi.
- Vanafunḏi vaandike kiṯabuni

**Majibu alopenḏekedhwa:**

**A**

1. Maradhi
2. Choo
3. Madhingira
4. Kukusanywa
5. Kipindrupindru

**B**

1. sabuni
2. kukota
3. mafucha
4. nsuaki
5. kitana

# 5 USALAMA

## ISOMO LA KWANḎA

### MAḎA KURU: KUSIKIDHA

### MAḎA NDRODI: KUSIKIDHA MAAGIDHO

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**:

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe;

- Kusikidha maagidho kwa makini
- Kudhingaṯia usalama
- Kufurahia kuunḏama maagidho

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk. wa 23

**Dhifaa dha kufundrishia:** Dhifaa halisi (kisu, sinḏanu), kifaa cha kidijitali

**Swali ḏaḏisi:** Uṯachumia mbinu gani kudhivia ajali?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha:**

- Changulidha kipindri kwa kuvavulidha vanafunḏi maswali kuhusu usalama.
- Vaagidhe vanafunḏi vafungue kiṯabu uk. wa 23 na vasikidhe maagidho a mwalimu.
- Vashirikishe vanafunḏi vaenge picha na vanene vavonacho.
- Kachika dhikundri vanafunḏi vajadiliane mbinu dha kudhivia ajali
- Hitimisha kwa kuchilia nkadho mbinu mbalimbali dha kudhivia ajali.

## ISOMO LA PILI

## MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA

### MAḎA NDRODI: KUSIMULIA DHISA

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**:

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

- Kusimulia dhisa kwa ufasaha
- Kufurahia kusikidha dhisa

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk. wa 24

**Dhifaa dha kufundrishia:** Picha Kiṯabuni

**Swali ḏaḏisi:** Kwa nini wapenḏa kusimulia hadisi?

Kwa nini wapenḏa kusikidha hadisi?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha:**

- Changulidha isomo kwa kudhungumudhia kuhusu usalama. Vavulidhe vanafunḏi vachaye mbinu dha kudhivia ajali.
- Vanafunḏi vafungue kiṯabu ukurasa wa 24, Vajadili picha.
- Vasimulie kisa kifupi kuhusu ajali
- Vashirikishe vanafunḏi vasimulie dhisa vadhiivadho kuhusu ajali
- Hitimisha isomo kwa kusisiṯidha asari dha ajali na vipi chuṯadhiepuka.

## ISOMO LA CHACHU

## MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA

### MAḎA NDRODI: WIMBO

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**:

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

- Kusoma shairi kuhusu usalama

- Kukariri shairi kuhusu usalama

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi uk wa 25

**Dhifaa dha kufundrishia:** Chati

**Swali ḏaḏisi:** Wimbo husaidia vipi kutoa ujumbe?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha:**

- Changulidha isomo kwa kuvaeledha vanafunḏi umuhimu wa usalama.
- Angika chati na uvaambie vanafunḏi vajadili kimakundri.
- Vaagidhe vanafunḏi vafungue kiṯabu uk. wa 25 vasome wimbo kwa sauti.
- Mwalimu aeledhe ujumbe ulioko kweṉe wimbo hoo.
- Vashirikishe vanafunḏi vaimbe wimbo hoo kwa mahadhi.

## ISOMO LA IṈE

## MAḎA KURU: KUSOMA

## MAḎA NDRODI: HAḎISI

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**:

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

- Kusoma haḏisi kwa ufasaha
- Kujibu maswali
- Kufurahia kusoma haḏisi

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi uk wa 26.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Picha kiṯabuni

**Swali ḏaḏisi:** Muhusika kachika haḏisi ni nyani?

Hupachae ujumbe kachika haḏisi?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha:**

- Changulidha kipindri kwa kuvavulidha vanafunḏi vaeledhe kisa chochote ambacho vameshuhudia kuhusu ajali.
- Vambie vafungue kiṯabu cha mwanafunḏi ukurasa wa 26, vakiva vavilivavili vaongodhe kuijaḏili picha iliyoko kiṯabuni.
- Vape muda wa kuisoma haḏisi hio kwa makundri kisha uṯaue baadhi avo vasome kwa sauṯi darasani kila mmoya aya moya.
- Vape muḏa vajaḏili maswali a haḏisi kisha kila mmoya aanḏike majibu kachika dhiṯabu dhavo.

## ISOMO LA ṮANU

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

**MAḎA NDRODI: KUANḎIKA SENCHENSI**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**:

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

- Kuanḏika senchensi kuchumia nchoro.
- Kusoma senchensi
- Kufurahia kuanḏika senchensi.

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk wa 28

**Dhifaa dha kufundrishia:** chati, kadi-maneno

**Swali ḏaḏisi:** Michoro husaidia vipi? Usalama una umuhimu gani?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha:**

- Changulidha isomo kwa kueledhea umuhimu wa kudhingaṯia usalama
- Vambie vafungue kiṯabu cha mwanafunḏi ukurasa wa 28, vaongodhe kujaḏili picha kiṯabuni.
- Vavoneshe kadi dha maneno, vanafunḏi vadhisome kisha vaagidhe vachunge senchensi.

- Vape muda kujadili tena picha kiṯabuni na vachunge senchensi kuchumia michoro.

## ISOMO LA SIṮA

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

## MAḎA NDRODI: KUPANGA SENCHENSI

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

- Kupanga senchensi kupacha kifungu sahihi.
- Kusoma senchensi

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ukurasa 29

**Dhifaa dha kufundrishia:** Chati

**Swali ḏaḏisi:** Wadhingatia nini upangapo senchensi ili upache kifungu sahihi?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Changulidha isomo kwa kuangika chati ubavoni ilo na senchensi.
- Vaagidhe vanafunḏi vasome senchensi kwa sauṯi.
- Vaambie vafungue kiṯabu cha vanafunḏi ukurasa wa 29 vaagidhe vasome senchensi.
- Vaeledhe vaṯakavopanga senchensi kwa ufasaha ili vapache kifungu sahihi.
- Hiṯimisha isomo kwa kuvashirikisha vanafunḏi vasome kifungu valichokipanga kwa sauṯi.